HOTUBA YA MGENI RASMI KATIKA SHEREHE ZA KUADHIMISHA SIKU YA KUTOKOMEZA UTUMIKISHWAJI WA WATOTO NA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA:

Ndugu;
Mkurugenzi Mtendaji
Waheshimiwa Madiwan
Wakuu wa idara
Viongozi wa Dini
Wawakilishi wa Asasi zisizo za kiserikali
Mabibi na Mabwana

Asalaam aleikhum, Bwana Yesu asifiwe, tumsifu Yesu kristo.

Ndugu wananchi
Kwanza kabisa nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa fursa hii ya kujumuika nanyi leo katika tukio hili muhimu kwetu sote la kuadhimisha siku ya **Kutokomeza Utumikishwaji wa Watoto**, lakini vile vile **Siku ya Mtoto wa Afrika** ambapo kama mjuavyo kila mwaka ifikapo tarehe 12 Juni, dunia huadhimisha siku ya Kutokomeza Utumikishwaji watoto na vile vile kila mwaka tarehe 16 Juni nchi za Afrika huadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika.

Kwa kuwa siku hizi mbili tofauti yaani siku ya KUTOKOMEZA UTUMIKISHWAJI WA MTOTO NA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA zote huadhimishwa katika wiki hii, na kwa kuwa siku hizi zote mbili zina mlenga mtoto, imekuwa ni jambo jema kufanya maadhimisho haya kwa pamoja.
Aidha napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa shirika la Winrock International kupitia Mradi wa ARISE kwa kushirikiana na Halmashauri kuandaa maadhimisho haya kwa pamoja.

Ndugu wananchi;
Siku ya kutokomeza utumikishwaji watoto duniani ni matokeo ya azimio la shirika la kazi duniani (ILO) lililopititishwa mwaka 2002, ambapo nchi mbali mbali duniani ikiwepo Tanzania zime ridhia azimio la Shirika la Kazi Duniani (ILO) nambari 138 [1] juu ya kiwango cha umri wa chini wa ajira kwa Watoto na vile vile mkataba wa ILO namba 182 [2] juu ya aina mbaya zaidi ya kazi za ajira kwa watoto. yaani, (worst forms of child labour).Hivyo, tangu hapo kila mwaka ifikapo Juni 12, dunia huadhimisha siku hii kwa lengo la kuendeleza mapambano na vuguvugu la **Kutokomeza Utumikishaji Watoto** ambapo siku hii hutumika kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara na athari mbali mbali ambazo watoto chini ya umri wa miaka 18 huzipata kwa kufanya kazi ambazo hazilingani na umri wao kama vile; Kuwanyima watoto fursa ya kupata elimu; Kuwanyima watoto

haki yao ya utoto kwa kuwapa majukumu ambayo hayaendani na umri wao kama kuzalisha mali; na Kuwasababishia madhara ya kiafya, kimwili na kisaikolojia.

Ndugu wananchi;
Siku ya mtoto wa Afrika imetokana na Azimio la nchi 51 za Afrika wanachama wa OAU LA mwaka 1991 ,ilitokana na mauaji ya kikatili ya watoto waliokuwa wanaishi katika kitongoji cha **SOWETO** nchini Afrika Kusini mnamo mwaka 1976.Lengo la siku hii ni kuwapa fursa watoto wote wa bara letu la Afrika kuungana kutetea haki zao(
Ndugu wananchi;
Kama ilivyo ada, siku hii kila mwaka huadhimishwa kwa kauli mbiu maalum; na kauli mbiu ya mwaka huu inasema; **"Tuungane pamoja kutokomeza Utumikishaji Watoto".** Na kauli mbiu ya kitaifa ya mtoto wa Afrika inasema **" Maendeleo Endelevu 2030: *i*marisha Ulinzi na Fursa sawa kwa Watoto Wote"** Hivyo, kwa kauli mbiu hizi napenda kuchukua fursa hii kuwaasa wananchi wote kwa pamoja tuungane kupinga Utumikishaji Watoto wetu na badala yake tuwape watoto fursa ya kufanya yale wanayo paswa kufanya watoto kama vile kwenda shule, kucheza pamoja na kupewa haki zao zote za msingi na kulindwa.

Aidha nataka kuwakumbukusha kwamba suala hili sio la hiari kwa kuwa sheria zetu za nchi mfano sheria ya Ajira na Mahusiano ya kazini namba 6 ya Mwaka 2004, Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 na Sheria ya Usafirishaji Binadamu Namba 6 ya mwaka 2008 zote zimekataza jambo hili. Hivyo, kutokana na sheria hizi, ni wazi kuwa kumtumikisha mtoto chini ya umri uliowekwa na sheria na vile vile kuwafanyisha watoto kazi zilizotajwa na sheria kuwa ni kazi mbaya kama vile kufanya kazi kwenye mashamba ya tumbaku ni kosa la jinai

Ndugu wananchi, mbali na makatazo yote haya idadi ya watoto wanaotumikishwa inaendelea kuongezeka kutokana na serikali za vijiji na jamii kushindwa kusimamia na kutekeleza sheria na makatazo hayo. Ni lazima ifahamike kuwa sambamba na kuvunja sheria, lakini vile vile makampuni ya tumbaku yanapinga watoto kushiriki katika uzalishaji wa tumbaku kwa kuwa si jambo sahihi na zimekuwa zikitoa elimu kwa Wakulima kupitia miradi kama ARISE, program ya masharti ya kilimo cha tumbaku, yaani Agriculture Labour Practices (ALP) n.k.

Kama ilivyo elezwa, Elimu duni miongoni mwa jamii ya kutokujua haki za watoto na umaskini uliokithiri ni vyanzo vikubwa vinavyosababisha kutumikishaji wa watoto. Uchunguzi umebaini kuwa pamoja na watoto kutumikishwa kazi kwa ujira mdogo lakini hata hivyo ujira wake hupokelewa na wazazi au walezi na mtoto kubaki akifanya kazi huku akiambulia chakula na nguo kuukuu (zilozochakaa) kutoka katika familia au mwajiri.

Katika msimu wa kilimo kwa zao la tumbaku pekee imethibitika kwamba mtoto hutumikishwa katika shughuli mbalimbali kama vile;

- ✓ Kuandaa vitalu au mabedi, Kumwagilia mbegu, Kung'olea magugu, Kuhamisha miche

- ✓ Kungoa miche ya tumbaku kwenda shambani, Kupanda miche shambani, Kusomba kuni na kuzikata
- ✓ Kuweka mbolea shambani, Kupalilia mashamba ya tumbaku
- ✓ Kuchuma tumbaku, Kubeba majani ya tumbaku kupeleka kwenye mabani
- ✓ Kuchochea moto, Kusuka majani ya tumbaku, Kuchambua tumbaku na Kupanga tumbaku

Na kazi nyingine nyingi ambazo zote hizi sheria imezitaja kama kazi mbaya na hatarishi kwa watoto.
Wengi tunafahamu athari za utumikishwaji watoto kwenye mashamba ya tumbaku ikiwa ni pamoja na kukosa elimu, lakini ni wachache wanaofahamu madhara ya kiafya, kisaikolojia na kimakuzi wanayoyapata watoto wetu, hivyo ni wajibu wetu kuwasikiliza wataalamu ili muweze kuchukua tahadhali

Ndugu wananchi, Kwa sababu hiyo, napenda kutumia fursa hii pamoja na kutoa elimu juu ya jambo hili, pia napenda kutoa onyo kwa wazazi na familia ambazo hushiriki katika kuvunja sheria hizi za nchi. Serikali haita vumilia kuendelea kuona kwamba watoto wanakosa shule kwa sababu ya kushiriki kwenye shughuli za mashamba ya tumbaku na Kuchunga mifugo.

Ndugu wananchi;
Ni kweli kabisa kuwa UTUMIKISHWAJI wa Watoto bado ni tatizo kubwa nchini na hasa katika wilaya yetu hii. Takwimu za kitaifa zinaonyesha kwamba kati ya watoto watatu (3) wenye umri wa miaka 5 - 17, mtoto mmoja anafanya kazi ambazo ni hatarishi katika maisha yake kiafya, kimwili na kisaikolojia.

Mfano, kwa mujibu wa utafiti wa Utumikishwaji wa watoto wa mwaka 2014 ambao ni wa tatu kufanyika nchini ambapo utafiti wa kwanza ulifanyika mwaka 2001 na wa pili ulifanyika mwaka 2006, Matokeo ya Utafiti huo yameonyesha kuwa, kati ya watoto milioni 15 wenye umri kati ya miaka 5 – 17, watoto milioni 4.2 sawa na asilimia 28.8 wanatumikishwa katika kazi mbalimbali za kiuchumi.

Utafiti huu umebainisha kuwa, watoto wanafanya kazi zaidi katika sekta za Kilimo, Misitu na Uvuvi ambazo zinaajiri asilimia 92.1 ya watoto wote wanaojishughulisha na shughuli za kiuchumi.

Aidha utafiti huo umebainisha pia, kwamba shughuli za kujisomea kwa watoto ni asilimia ndogo sana ambapo wavulana wanatumia muda mrefu zaidi kujisomea kwa asilimia 16.4 tu na wasichana hutumia asilimia 14.6 tu ya muda wao kujisomea jambo ambalo linachangia matokeo mabaya katika mitihani kwa watoto wetu.

Aidha, matokeo pia yameonesha kuwa utumikishwaji ni mkubwa kwa watoto wasiosoma ikilinganishwa na watoto wanaosoma. Na kwamba, matokeo yameonesha utumishwaji ni mkubwa katika maeneo ya vijijini ikilinganishwa na maeneo ya mjini.

Utafiti huu umebainisha viashiria vya hali ya watoto wanaofanya kazi za kiuchumi na zisizo za kiuchumi, hali ya utumikishwaji wa watoto pamoja na athari mbalimbali ambazo watoto wanapata kwa kujihusisha na shughuli mbalimbali za utumikishwaji.

Ndugu wananchi,
Kama ilivyo elezwa hapo awali, miongoni mwa sababu nyingi za kuwatumikisha watoto ni umaskini wa kipato, Ukosefu wa elimu kwa jamii, lakini vile vile idadi kubwa ya watoto na umaskini uliokithiri kwa jamii. Hata hivyo sababu hizo sio kinga ya kuvunja sheria kwa kuwatumikisha watoto kinyume na taratibu, sheria, miongozo ya malezi na makuzi ya watoto wetu.

Ndugu wananchi; hapa nataka niweke wazi na ieleweke kuwa, kuendelea kuwepo kwa vitendo vya utumikishwaji watoto unaofanywa hasa katika kilimo cha tumbaku ndani ya vijiji vyenu ni ukiukwaji wa sheria za nchi zinazokataza ajira kwa watoto. Lakini, pia vile vile narudia kusema tena ifahamike kwamba kampuni zinazo fanya biashara ya Tumbatu hapa nchini na kote duniani vile vile zinakataza na zisingependa kununua tumbaku ambalo linazalishwa kwa kutumia nguvu kazi ya watoto.

Ndugu wananchi;
Nimeambiwa mradi huu wa ARISE unakusudia kufanya kazi na jamii kuondoa utumikishaji wa watoto kupitia elimu na kuwawezesha wan-ajamii kukabiliana na changamoto za umasikini kama vile kubuni na kutekeleza miradi midogo midogo ya kuinua kipato kwa makundi ya vijana na akina mama. Mradi huu wa ARISE umekuja muda muafaka kwetu, kwani wananchi wengi hasa wakulima wangependa kufahamu masuala ya watoto (kuhusu haki, Malezi, wajibu na utumikishwaji) namna yanavyoathiri maisha yao ya kila siku na namna wanavyoweza kukabiliana na tatizo la umasikini kwa kupata elimu ya ujasiliamali (entrepreneurship) n.k.

Nataka niwahamasishe wananchi wote na hasa familia zilizo katika mazingira hatarishi kuitumia vema fursa hii chini ya shirika la Winrock International kupitia Mradi huu wa ARISE.

Sisi kwa upande wa uongozi wa wilaya pamoja na Halmashauri ya wilaya kwa maana ya ofisi ya Mkuu wa wilaya na Mkurugenzi, tumeupokea mradi huu kwa mikono miwili na tutahakikisha kuwa tunatoa mchango wetu ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyo kusudiwa.

Sasa nataka nitoe agizo kwa mara nyingine hapa viongozi wa serikali za vijiji na viongozi wa kata kujipanga vizuri katika kuhakikisha mpango wa ARISE unafanikiwa. Kama mtakumbuka vizuri hapo nyuma niliwahi kutoa agizo kama hili hapa ***kijijini Itebulanda***

tarehe 25/10/2016 siku ya mkutano wa kuunda Kamati ya Kutokomeza Utumikishaji wa Watoto ya Kijiji hiki.

Vile vile, nataka niwaombe wananchi wa kijiji hiki na vijiji vyote ndani ya kata na wilaya yangu kwa ujumla, tuwape ushirikiano wa kutosha shirika la Winrock International katika juhudi za kusaidia mradi huu wa ARISE katika utekelezaji na utokomezaji utumikishaji watoto.

Kwa hakika mradi huu ukitekelezwa vizuri ambao tutanufaika zaidi ni sisi watu wa Urambo hususani hapa Itebulanda. Hivyo, tushiriki kwenye shughuli za mradi na tuthubutu kujaribu njia mpya na bora za kilimo cha tumbaku ambazo hazihusishi watoto

Ndugu viongozi na wananchi kwa ujumla;
Kwa upande wa watendaji wa serikali na wadau wengine, ni wakati sasa na sisi wa serikalini kujipanga na kuhakikisha sheria ya Mtoto namba 21 ya 2009, sera ya mtoto na miongozo mbalimbali inasimamiwa kikamilifu ili kuhakikisha kuwa utumikishwaji wa watoto hautokei na kufanyika katika maeneo yetu.

Ndugu wananchi;
Mwisho: Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wenzetu wa nchi ya Japani kupita kampuni ya JTI kwa kufadhili mradi huu wa ARISE, ambapo ni mradi muhimu kwetu kwa mustakibali wa watoto na taifa letu. Kwani bila kuwapa fursa watoto kwenda shule na kubakia kufanya kazi za tumbaku kwa hakika tutaendelea tutajenga jamii na taifa la watu masikini.

Kwa namna ya kipekee kabisa nikupongeze wewe Bwana Magawa Abdallah, Mkurugezi wa Mpango huu wa ARISE Tanzania na timu yako kutoka shirika la Winrock International kipekee kwa maandalizi na kufanikisha maadhimisho haya. Aidha nikupongeze Mkurugenzi wa Halmashauri yetu ya Urambo na timu Kamati ya wilaya ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwa Ushirikiano wenu na shirika la Winrock International

Naomba niupongeze uongozi wa Kijiji na Kata na Wananchi wote kwa ujumla kwa kuhakikisha kwamba maadhimisho haya yanafana, bila kuwasahau Walimu na watoto walioshiriki katika michezo mbalimbali.

Mwisho kabisa, naomba niwatakie heri wananchi wote mlio shiriki katika mkutano huu. Kwa wale ambao wametoka nje ya kata na wilaya hii nawatakia heri na safari njema mkiwa mnarejea makwenu.

Naomba sasa nitangaze rasmi kuwa maadhimisho haya yamefunguliwa rasmi. Nataka niwatakie heri kila mmoja atakaeshiriki kwa namna moja au nyingine katika utekelezaji wa mradi huu.

---------- Asanteni sana kwa kunisikiliza----------